

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

03

MAARIFA YA JAMII

Muda: Saa 1:30

Alhamisi, 21 Novemba 2019

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A na B zenyе jumla ya maswali **manne** (4).
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.

SEHEMU A: (Alama 28)

1. Jibu kipengele cha (i) – (viii) kwa kuchagua **herufi ya jibu sahihi** na kuiandika kwenye kisanduku.
 - i. Bwana Juma huishi na mkewe, watoto wawili na dada yake. Hii ni aina gani ya familia?
A. Familia ya awali C. Familia pana.
B. Familia ya mzazi mmoja. D. Familia ya makubaliano. []
 - ii. Migogoro kati ya wakulima na wafugaji husababishwa na _____
A. Vyama vingi vya siasa C. Uhaba wa mifugo na mazao.
B. Uhaba wa ardhi D. Kupungua kwa wafugaji. []
 - iii. Dada wa baba yangu huitwa?
A Mama B Bibi. C Shangazi. D Dada. []
 - iv. Kwanini tunawakumbuka viongozi wetu wakuu wa nchi ya Tanzania wa zamani?
A. Walituletea amani na umoja C. Walituletea utawala wa kigeni.
B. Walituletea fedha za kutosha D. Walituletea mifarakanano []
 - v. Ni sera gani kati ya hizi iliasisiwa na Rais wa zamani Ali Hassan Mwinyi?
A. Ujamaa na Kujitegemea C. Elimu bure kwa wote
B. Soko huria. D. Ubinafsishaji. []
 - vi. Zifuatazo ni hasara za uhusiano mbaya wa wanafunzi shulen,
isipokuwa:
A. Kuchukia masomo C. Kutengeneza maadui shulen.
B. Kutoweka kwa amani shulen. D. Kukuza mshikamano shulen
 - vii. Ni kundi lipi la jamii za Kitanzania bado linaendeleza mfumo wa ujima?
A. Wandorobo, Wasandawe, na Wamakonde.
B. Wamasai, Wasandawe, na Wafipa.
C. Wahadzabe, Wandorobo, na Wakurya.
D. Wandorobo, Wasandawe na Wahadzabe. []
 - viii. Moja ya faida tunayoipata kwa kucheza ngoma za utamaduni ni
A. Kuendeleza utandawazi C. Kukuza mila na desturi.

2. Jibu kipengele cha (i) hadi (vi) kwa kuoanisha maelezo ya fursa mbalimbali kutoka **Fungu A**, na aina husika ya fursa husika kutoka **Fungu B**.

Na.	Fungu A	Herufi	Fungu B
i.	Fursa zilizopo kwenye maeneo yenye mbuga za wanyama.		A. Kilimo B. Mbao
ii.	Fursa zilizopo maeneo yenye misitu.		C. Madini D. Uashi
iii.	Fursa zilizopo maeneo yenye rutuba na mvua nyingi.		E. Ufundii F. Ufugaji
iv.	Fursa zilizopo maeneo yenye uwanda wa nyasi.		G. Utalii H. Uvubi
v.	Fursa zilizopo maeneo yenye mito, maziwa na bahari.		

SEHEMU B: Maswali ya Majibu Mafupi

3. Soma kifungu cha habari na kisha jibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho.


Hali ya joto au baridi ya sehemu au kitu huitwa jotoridi. Kifaa kinachotumika kupima jotoridi huitwa kipimajoto. Chanzo cha cha joto ni juu. Kunapokuwa na joto kali tunasema jotoridi liko juu lakini kunapokuwa na baridi tunasema joto liko chini. Kunapokuwa na baridi tunashauriwa kuva nguo nzito kama sweta na jaketi. Wakati wa joto kali tunavaa nguo nyepesi au nguo za pamba. Hali ya joto husababisha mito na mabwawa kukauka.

Maswali:

- i. Hali ya joto au baridi ya mahali huitwaje? _____
- ii. Mavazi gani huvaliwa wakati wa baridi? _____
- iii. Ni katika hali gani jotoridi huwa juu? _____
- iv. Kifaa kinachotumika kupima jotoridi huitwa? _____
- v. Chanzo cha jotoo ni nini? _____
- vi. Mito na mabwawa hukauka wakati gani? _____
- vii. Nguo nyepesi na za pamba huvaliwa wakati gani? _____

4. Soma kwa makini ramani ya kijiji cha Mtakuja uliyopewa, na kisha jibu vipengele vilivyoulimiza kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizo wazi.

Ramani ya kijiji cha Mtakuja



Ufunguo

	Kanisa
	Msikiti
	Bwawa
	Msitu
	Mlima
	Shule
	Kiwanda cha chai
	Kiwanda cha mbao
	Josho
	Machimbo
	Makazi ya watu
	Daraja
	Kisima

Maswali:

- i. Kuna madaraja mangapi katika ramani? _____
- ii. Kuna milima mingapi katika ramani? _____
- iii. Kuna visima vingapi katika ramani? _____
- iv. Mto B unamwaga wapi maji yake? _____